

Taarifa ya Faragha ya Worldcoin

Ilisasishwa mwisho: Agosti 25 2022

Asante kwa kuchagua kuwa sehemu ya Jumuiya ya Worldcoin!

Taarifa hii ya Faragha inashughulikia data unayotupatia kuitia matumizi yako ya tovuti, programu Worldcoin', itifaki, na huduma zingine zilizounganishwa na Taarifa hii ya Faragha (kwa pamoja, "Huduma"). Taarifa hii ya Faragha imejumuishwa na kusimamiwa na Sheria na Masharti ya Mtumiaji ya Worldcoin (worldcoin.org/tos). "Worldcoin" inamaanisha Tools for Humanity Corporation na kampuni zake tanzu zinazomilikiwa kikamilifu na Tools for Humanity GmbH.

Ili kupata maelezo kuhusu jinsi tunavyokusanya, kutumia, kuhifadhi, na kufuta data zako za bayometriki zilizokusanya kuitia Orb yetu, tafadhalii pitia [Fomu ya Idhini ya Data](#), iliyojumuishwa kama rejeleo. Hatutakusanya data zako za bayometriki isipokuwa uwe umekubaliana na [Fomu ya Idhini ya Data](#).

Sheria ya Faragha ya Mteja ya California, kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Haki za Faragha ya California, haitumiki kwa Worldcoin kwa sasa.

1. Sasisho za Kauli hii ya Faragha

Wakati mwengine tunasasisha Kauli hii ya Faragha. Tukifanya mabadiliko makubwa, kama vile jinsi tunavyotumia maelezo yako ya kibinagsi, basi tutakuarifu kuitia baruaopepe au ujumbe katika app yako ya Worldcoin.

2. Je, Kauli hii ya Faragha inajumuisha nini?

- Ahadi yetu ya kulinda faragha yako na data zako
- Taarifa tunazokusanya na kwa nini
- Jinsi tunavyotumia data tunazokusanya
- Mahali ambapo tunachakata data zako
- Wakati ambao tunashiriki data zako
- Jinsi data zako zinavyorekodiwa kwenye blockchain ya umma
- Jinsi tunavyotumia vidakuzi
- Muda tunaohifadhi data zako
- Jinsi Kauli hii ya Faragha ilivyo tofauti kwa watoto na vijana
- Jinsi ya kuwasiliana nasi kuhusu Kauli hii ya Faragha
- Haki za kisheria ulizonazo chini ya GDPR

3. Ahadi yetu ya Kulinda Faragha yako na Data zako

Worldcoin inawajibika kwenye mchakato wa data yako ya kibinagsi. Unaweza kuwasiliana na Worldcoin kuitia Tovuti yetu ya Ombi kwa worldcoin.org/requestportal au kwa 548 Market Street, PMB 49951, San Francisco, CA 94104 USA.

Tunajitahidi kwa dhati kulinda faragha yako na kulinda data yako. Katika Worldcoin, tunatambua kwamba tunaweza tu kutimiza dhamira yetu ya kusambaza Worldcoin kwa njia ya haki kwa watu wengi kadri iwezekanavyo ikiwa watu watakuwa na imani nasi, na faragha na usalama wa data ni jambo la msingi ili kupata imani yako.

Faragha

Tumebuni bidhaa na huduma zetu tukizingatia faragha yako. Sisi hukusanya data ili kuboresha bidhaa na huduma zetu.

Tutakuambia kila wakati, hapa katika Taarifa hii ya Faragha au katika fomu za idhini ya data kwa bidhaa au huduma maalum, ni data gani tunakusanya, kwa nini tunaikusanya, na tunachofanya nayo.

Usalama wa Data

Tumeteua timu ya kutunza data zako na tumeweka kinga halisia na za kielektroniki zinazolinda data zako zinaposafirishwa na zinapohifadhiwa. Wakati huo huo, hakuna huduma inayoweza kuwa salama kabisa. Ikiwa una wasiwasi wowote kuhusu akaunti yako au data zako, tafadhali wasiliana nasi kuititia Lango letu la Maombi au kwa kututumia barua kwa anwani Tools For Humanity Corporation, 548 Market Street, PMB 49951, San Francisco, CA 94104 USA.

4. Maeleo Tunayokusanya na Kwa Nini

4.1 Data Unazotupatia

Wewe kama mtumiaji, hauhitajiki kupatiana data zozote ili kufikia programu ya Worldcoin. Hata hivyo, unaweza kuhitajika kutupatia data fulani ili uweze kutumia kipengele fulani ndani ya Huduma. Misingi ya kisheria ya kuchakatwa katika kesi zilizo hapa chini ni idhini ya mtumiaji' na utendakazi wa kandarasi, yaani kutoa Huduma. Hapa chini kuna orodha ya data unazoweza kupatiana na tunachowenza kufanya na data hizo:

- **Jina la kwanza na la mwisho:** Unaweza kuchagua kuweka jina lako ili kulihusisha na akaunti yako. Worldcoin pamoja na watumiaji wengine huenda wakaona jina lako wanapoamua kutangamana na akaunti yako. Huenda tukahitaji jina lako unapowasilisha ombi la data za mhusika.
- **Anwani ya baruapepe:** Unaweza kuchagua kuweka anwani yako ya baruapepe ili kuihusisha na akaunti yako. Huenda tukahitaji anwani yako ya baruapepe unapowasilisha ombi la data za mhusika.
- **Nambari ya simu:** Unaweza kuchagua kuweka nambari yako ya simu ili kuihusisha na akaunti yako. Kwa kibali chako, watumiaji wengine wanaweza kutafuta akaunti yako kwa kutumia nambari yako ya simu. Huenda tukahitaji nambari yako ya simu unapowasilisha ombi la data za mhusika.
- **Maoni na barua kutoka kwako:** Hii inajumuisha baruapepe zozote, ujumbe wowote, au mawasiliano mengine yoyote unayotutumia kuititia baruapepe au tovuti za mitando ya kijamii ya wahusika wengine.
- **Anwani za kitabu cha anwani:** Unaweza kururuhusu kufikia kitabu chako cha anwani ili kuwezesha kipengele ambacho kinakurahisishia kutafuta na kutangamana na watumiaji wengine ambao huenda wakawa katika kitabu chako cha anwani. Maeleo ya kitabu cha anwani yanásalia kwenye kifaa chako.

Tafadhali kumbuka: Una jukumu la kuhakikisha kwamba kushiriki maeleo yako' ya mawasiliano kunaambatana na sheria husika. Hii inaweza kuhitaji kupata ruhusa ya anwani zako.' Unaweza kubadilisha uamuzi wako na kuondoa uwezo wetu wa kufikia anwani zako wakati wowote katika mipangilio ya kifaa chako. Ukichagua kuingiza anwani za kitabu cha anwani' za kifaa chako kwenye Programu ya Worldcoin ili kujua ni nani kati ya watu unaowsiliana nao anatumia Huduma zetu au kuwaalika wajunge nawe katika kutumia Huduma zetu, tutasawazisha nambari zako za simu mara kwa mara' kwa nambari hizo na anwani zinazolingana za pochi zinazotolewa na watumiaji wengine kwenye seva zetu.

- **Maeleo ya Eneo.** Unaweza kuamua kuwasha huduma inayotegemea eneo (kama vile kipengele kinachokuruhusu kupata Mhudumu wa Orb karibu nawe). Tunaweza kukusanya taarifa kuhusu eneo lako kuititia GPS, anwani ya IP, maeleo ya mnara wa simu, au maeleo ya mahali pa kufikia Wi-Fi. Aina ya maeleo ya eneo yanayokusanywa inalingana na huduma unayotumia, kifaa unachotumia (kwa mfano, Apple au Android), na mipangilio ya kifaa chako (iwe vibali vimewezeshwa au kulemazwa). Unaweza kubadilisha vibali vyako wakati wowote katika mipangilio ya kifaa chako.
- **Data ya Biashara.** Ikiwa una uhusiano wa kibiashara nasi (kama vile wewe ni Mhudumu wa Orb au msambazaji), basi tunaweza kuhitaji maeleo kama vile majina, anwani ya barua, baruapepe, nambari ya

simu, anwani ya pochi, na nyaraka zingine (kama vile kitambulisho chako cha serikali) kama sehemu ya kuimarishe uhusiano huo wa kibashara na ili kutimiza majukumu ya kumjua-mteja-wako. Tunaweza kutumia huduma za watusika wengine, kama vile Onfido, ili kutusaidia kukusanya na kuhakiki maelezo na nyaraka zilizotajwa hapa juu ili kutimiza majukumu ya kumjua-mteja-wako.

4.2 Data Tunazokusanya Kutoka Kwa Vyano Vingine

Mara kwa mara, tunaweza kupata taarifa kukuhusu kutoka kwa vyano vifuatavyo nya watu wengine:

- **Data za Blockchain.** Tunaweza kuchambua data za blockchain ya umma ili kuhakikisha kwamba watu wanaotumia Huduma zetu hawajihusishi katika shughuli haramu au zilizopigwa marufuku chini ya Makubaliano yetu ya Mtumiaji wa Worldcoin, na ili kuchambua mitindo ya miamala kwa madhumuni ya utafiti na utengenezaji.
- **Huduma za Uthibitishaji wa Kitambulisho.** Tunaweza kupata maelezo kutoka kwa huduma za watusika wengine kwa kutumia data zako ili kuthibitisha utambulisho wako ikiwa inahitajika na sheria (kama vile mahitaji husika ya kumjua-mteja-wako). Ili kufanua, **hatutumii** data zako za bayometriki tunapothibitisha utambulisho wako kama inavyohitajika na sheria.

4.4 Data Tunazokusanya Kiotomatiki

Tukiruhusiwa chini ya sheria husika, tunaweza kukusanya aina fulani za data kiotomatiki unapotumia Huduma zetu. Maelezo haya yanatusaidia kuangazia masuala ya uhudumiaji wateja, kuimarishe utendakazi wa Huduma, kukupa huduma fanisi na ya kibinagsi, na ili kulinda maelezo ya kuingia kwenye Akaunti yako. Taarifa zilizokusanya kiotomatiki ni pamoja na:

- **Vitambulisho nya Mtandaoni:** Maelezo ya eneo la kijiografia (tazama hapa juu), mfumo msingi wa uendeshaji kompyuta au simu ya mkononi, jina na toleo la kivinjari, na anwani za IP
- **Data ya Matumizi:** Data ya uthibitishaji, maswali ya usalama, machapisho ya mitandao ya kijamii ya umma, na data nyingine iliyokusanya kuitia vidakuzi na teknolojia sawa.
- **Vidakuzi:** faili ndogo za data zilizohifadhiwa kwenye diskii kuu au kumbukumbu ya ndani ya kifaa ambazo hutusaidia kuboresha Huduma zetu na matumizi yako, kuona ni maeneo na vipengele vipi nya Huduma zetu ni maarufu, na vimetembelewa mara ngapi.

Hivyo hivyo, programu ya simu ya Worldcoin inakusanya maelezo kwa ajili ya usuluhishaji matatizo na uimarisaji. Tunatumia huduma za watusika wengine, kama vile Segment.io au PostHog, ili kufanya makadirio ya maelezo kuhusu matumizi ya watumiaji. Inapowezekana, tunachukua hatua ili kupunguza au kuficha maelezo yanayotumwa kwa watusika wengine (kama vile kusimba data).

Msingi wa kisheria wa kuchakata data iliyotajwa hapo juu ni maslahi halali ya programu au tovuti inayofanya kazi.

4.5 Data Bila Utambulisho na Zilizokadiriwa

Kuficha utambulisho ni mbinu ya kuchakata data ambayo hurekebisha data ya kibinagsi ili isiweze kuhusishwa na mtu maalum. Mifano ya data bila utambulisho zinajumuisha:

- Data za miamala
- Data za ubonyezaji maeneo ya skrini
- Vipimo nya utendakazi
- Viashiria ulaghai

Pia tunakusanya data, kwa kuchanganya kiasi kikubwa cha taarifa pamoja ili isimtambue tena au kurejelea mtu binagsi. Tunatumia data isiyojulikana au kujumlisha kwa madhumuni ya biashara yetu, kama vile kuelewa mahitaji na tabia

za mtumiaji, kuboresha Huduma zetu, kuendesha akili na masoko ya biashara, kugundua vitisho vya usalama na kufunza teknolojia zetu.

Msingi wa kisheria wa kuchakata data iliyotajwa hapo juu ni maslahi halali ya programu au tovuti inayofanya kazi, maarifa ya biashara na kuzuia ulaghai.

4.6 Data za Bayometriki

Tutakusanya tu na kutumia data zako za bayometriki baada ya wewe kukubaliana na [Fomu ya Idhini ya Data, ambayo inaelezea kwa kina aina za data za bayometriki tunazosindika na kwa nini](#). Data za bayometriki [hazijaunganishwa](#) na data za akaunti yako katika Sehemu ya 4 hapa juu.

Msingi wa kisheria wa kuchakata data iliyotajwa hapo juu ni idhini ya mtumiaji' ya wazi.

5. Jinsi Tunavyotumia Data Tunazokusanya

Ni lazima tuwe na sababu halali (au "msingi wa kisheria wa kusindika") ya kutumia maelezo yako za kibinafsi. Hata hivyo, wakati unatutarajia sisi kutumia maelezo yako ya kibinafsi na matumizi yetu ya maelezo hayo yanaambatana na sheria husika, hatukuombi kibali chako. Inapohusu data zako za bayometriki, tunakuomba idhini yako moja kwa moja.

Tunatumia maelezo yako kwa malengo yafuatayo:

- Kutoa, kudumisha, kuboresha na kuendeleza bidhaa na huduma zetu, ikijumuisha kutatua na kurekebisha hitilafu katika Huduma zetu;
- Kufanya utafiti ili kuimarisha na kuboresha bidhaa zetu;
- Kuzoesha teknolojia yetu ili iweze kutambua watumiaji binafsi vyema zaidi;
- Kuchambua matumizi yako ya Huduma zetu ili kukupa usaidizi bora;
- Kutumia anwani ya pochi lako ili kukutumia sarafu za Worldcoin tokens (WLD) au sarafu nyingine za kidijitali ambazo tunahusika nazo;
- Kuambatana na sheria husika (kama vile kutumia anwani yako ya IP ili kuwazuia watu binafsi kutoka mataifa au nchi zilizopigwa marufuku kutumia Huduma);
- Kushughulikia maombi, malalamishi na maswali yako;
- Kusuluuhisha migogoro, kutatua masuala, na kutekeleza makubaliano yetu nawe, pamoja na Kauli hii ya Faragha na Makubaliano ya Mtumiaji wa Worldcoin; na
- Kuwasiliana nawe kuhusiana na visasisho kwenye Huduma.

|

6. Mahali Ambapo Tunasindika Data Zako

6.1 Uhamisho wa Data.

Unapotupatia data zako, huenda zikatumwa, kuhifadhiwa, au kusindikwa katika eneo nje ya mahali ambako data zako zilikusanywa. Nchi ambayo data zako zinatumwa, kuhifadhiwa, au kusindikwa huenda zikawa hazina sheria za ulindaji data ambazo ni sawa na zile za nchi ambayo ulikuwa wakati ulipatiana data.

Tunatii kanuni zilizotajwa katika Sheria ya Jumla ya Ulinzi wa Data ya Umoja wa Ulaya' (GDPR), hata kama haihitajiki. Kwa mfano, wakati tunashirikiana na wasindikaji data wanaoendesha biashara yao nje ya Eneo la Kiuchumi la Ulaya (European Economic Area, EEA), tunahakikisha kwamba wanaambatana na GDPR. Tunashiriki tu data na wasindikaji data nje ya EEA ikiwa uhamishaji kama huo ni halali na ikiwa tuna uhakika kwamba msindikaji data huyo atalinda data yako inavyohitajika chini ya sheria zinazotumika na, zaidi, kwa mujibu wa viwango vya Worldcoin'. Tunapohamisha data kwa nchi ambayo

haina uamuza wa utoshelevu, tunatumia Vifungu nya Kawaida nya Mikataba nya EU.

6.2 Hatari za Uhamisho

Ifuatayo ni orodha ya hatari zinazoweza kutokea ikiwa tutahamisha data yako hadi Marekani, Umoja wa Ulaya au nchi nyingine:

- Ingawa tunafanya tuwezavyo ili kuhakikisha kwamba wakandarasi wetu wadogo wana wajibu wa kimkataba kulinda data yako ipasavyo, wakandarasi hawa wadogo wanaweza kuwa hawako chini ya sheria ya faragha ya data ya nchi yako. Ikiwa wakandarasi wadogo wangechakata data yako kinyume cha sheria bila idhini, basi inaweza kuwa vigumu kudai haki zako za faragha dhidi ya mkandarasi huyo mdogo.
- Inawezekekana' kwamba sheria ya faragha ya data katika nchi yako haipatani na sheria za faragha za data nchini Marekani au E.U.

Tafadhali kumbuka kuwa orodha hii ina mifano, lakini inaweza kuwa hajimuishi hatari zote zinazowezekana kwako.

6.3 HAKUNA KUPATIKANA KWA UTOVU WA SHERIA ZA FARAGHA ZA MAREKANI

Tume ya Umoja wa Ulaya, yenye jukumu la kufanya uamuza wa utoshelevu wa Sheria za Faragha za mamlaka nyingine kwa kulinganisha na GDPR bado hajjathibitisha vyema kuwa kiwango cha ulinzi wa data ya kibinagsi katika nchi hususa nchini Marekani, ambapo sehemu ya data yako inachakatiwa, hutoa kiwango sawa cha ulinzi kama Sheria za Faragha katika Umoja wa Ulaya.

7. Tunaposhiriki Data Yako

Hatutawahi kuuza data zako.

Wakati ambapo tunashiriki data zako nje ya Worldcoin, kila wakati:

- Tunazishiriki kwa njia salama;
- Tunahakikisha kwamba inashughulikiwa kwa njia ambayo inaendanisha na jitihada zetu kwa faragha yako; na
- Tunazuia kampuni zingine kutozitumia kwa malengo yao ya uuzaaji.

Tunashiriki data zako, na watu walio ndani ya Worldcoin na wale walio nje ya Worldcoin, kwa njia hizi chache:

- **Ndani ya Worldcoin:** Tunafichua data kwa washiriki wa timu ya Worldcoin pekee ambao wanahitaji ufikiaji ili kutekeleza majukumu na wajibu wao. Tunafichua tu kiwango cha data ambacho kinahitajika ili kufanya kazi na majukumu fulani.
- **Pamoja na wachuuzi na watoa huduma nje ya Worldcoin:** Tunafichua data kwa watoa huduma ambao huduma zao tunategemea ili kuchakata data na kukupa Huduma zetu. Tunafichua tu data kwa Wachuuzi wa Huduma ya Uthibitishaji Utambulisho ikiwa inahitajika na Sheria (yaani, mahitaji-ya-kumjua-mteja-wako). Data tunazowapatia Wachuuzi wa Huduma ya Uthibitishaji Utambulisho hazijumuishi data za bayometriki.
- **Pamoja na watekelezaji sheria, maafisa, au wahusika wengine:** Tunaweza kufichua data yako ili kutii sheria zinazotumika na kujibu madai ya lazima ya kisheria. Kwa uangalifu tunazingatia kila ombi ili kubaini kana kwamba ombi hilo linaambatana na sheria, na inapohitajika tunapinga maombi ambayo si halali, yanayopita mipaka, au yasiyo ya kisheria. Tunaweza kushiriki data ya kibinagsi na polisi na mamlaka nyingine za serikali ambapo tunaamini kuwa ni muhimu kutii sheria, kanuni au mchakato au wajibu mwininge wa kisheria.
- Tunaweza kushiriki maelezo yako ya kibinagsi ikiwa tunaamini kwamba vitendo vyako haviendani na makubaliano au sera zetu za watumiaji, ikiwa tunaamini kwamba umekiuka sheria, au ikiwa tunaamini kuwa ni muhimu kulinda haki, mali na usalama wa Worldcoin, watumiaji wetu, umma, au wengine.

- Tunaweza kushiriki maelezo yako ya kibinafsi na wanasheria wetu na washauri wengine wa kitaalamu inapohitajika ili kupata ushauri au vinginevyo kulinda na kusimamia maslahi yetu ya biashara.
- Tunaweza kushiriki maelezo yako ya kibinafsi kuhusiana na, au wakati wa mazungumzo kuhusu, muunganisho wowote, uuzaaji wa mali ya kampuni, ufadhili, au upataji wa yote au sehemu ya biashara yetu na kampuni nyingine.
- Data, ikijumuisha maelezo yako ya kibinafsi, inaweza kushirikiwa kati na mionganoni mwa Worldcoin na washirika wa sasa na wa baadaye, wafadhili, na kampuni tanzu na makampuni mengine yaliyo chini ya udhibiti na umiliki wa pamoja.
- Tunaweza kushiriki maelezo yako ya kibinafsi kwa idhini yako au kwa maelekezo yako.
- Pia tunaweza kushiriki habari iliyojumlishwa, isiyojulikana, au kutokutambuliwa ambayo haiwezi kutumika kukutambulisha.

8. Jinsi Data Zako Zinavyorekodiwa kwenye Blockchain ya Umma

Maelezo ya muamala yanayohusiana na matumizi yako ya Huduma za Worldcoin' yanaweza kurekodiwa kwenye blockchain ya umma.

Tafadhali kumbuka: Blockchains ni leja za umma za miamala ambazo hudumishwa kwenye mitandao iliyogatuliwa inayoendeshwa na wahusika wengine ambayo haidhibitiwi au kuendeshwa na Worldcoin. Kwa sababu ya hali ya umma na isiyoweza kubadilika ya leja za blockchain, hatuwezi kukuhakikishia uwezo wa kurekebisha, kufuta, au kudhibiti ufichuaji wa data ambayo hupakiwa na kuhifadhiwa kwenye blockchain, ikijumuisha IrisCode yako

9. Jinsi Tunavyotumia Vidakuza

Tunatumia vidakuza ili kusaidia Huduma zetu kufanya kazi vyema zaidi. Kando na vidakuza, tunaweza kutumia teknolojia nyingine sawa na hiyo, kama vile web beacons, ili kuwafuatalia watumiaji wa Huduma zetu. Web beacons, (pia zinaitwa "clear gifs") ni grafiki ndogo sana zilizo na kitambulishi cha kipekee, zilizo na utendaji sawa na vidakuza. Sera **Yetu ya Vidakuza**, imejumuishwa humu kwa marejeleo.

Worldcoin pia hutumia Google Analytics. Maelezo zaidi kuhusu jinsi Google hutumia data yako unapotumia tovuti na programu washiriki' wenzake, tembelea: <https://www.google.com/policies/privacy/partners/>. Kutumia Huduma hizi ni dhihirisho la idhini yako kwa Worldcoin ya kuhifadhi na kufikia vidakuza na data nyingine kwenye kompyuta yako au kifaa chako cha mkononi na Worldcoin' kutumia huduma ya Google Analytics kuhusiana na shughuli hizo. Tafadhali soma maelezo kwenye kiungo kilichotolewa ili uelewe kile unachokubali.

10. Tunahifadhi Data Zako Kwa Muda Gani?

Tunahifadhi data zako kwa muda ambao unahitajika ili kukupa Huduma zetu, kutimiza malengo yetu ya kibashara, na kuambatana na majukumu yetu ya kisheria na kudhibiti. Ukifunga akaunti yako nasi, tutafuta data ya akaunti yako ndani ya siku 90; au tutafuta data ya akaunti yako baada ya miaka 2 ya kutotumika. Ikihitajika kisheria, tutaendelea kuhifadhi data yako ya kibinafsi inapohitajika ili kutii wajibu wetu wa kisheria na udhibiti, ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa ulaghai, kutambua na kuzuia, pamoja na wajibu wa kodi, uhasibu na kuripoti wajibu wa kifedha. Ikiwa ungependa tufute data yako ya kibinafsi, ikijumuisha maelezo yako ya kibayometriki, basi tafadhali rejelea Sehemu ya 13 hapa chini.

Tafadhali kumbuka: Blockchain ni mitandao ya wahusika wengine ambayo haina mamlaka kuu na ambayo haidhibitiwi wala kuendeshwa na Worldcoin. Kwa ajili ya hali ya teknolojia ya blockchain kuwa ya umma na isiyoweza kubadilishwa, hatuwezi kurekebisha, kufuta, wala kudhibiti ufichuaji wa data zilizohifadhiwa kwenye blockchain.

11. Jinsi Kauli hii ya Faragha ilivyo Tofauti kwa Watoto na Vijana

Watu walio na umri wa chini ya miaka 18 hawaruhusiwi kutumia Huduma, na hatukusanyi data kutoka kwa watu walio chini ya umri wa miaka 18 kimakusudi. Iwapo unaamini kwamba mtoto wako aliye chini ya umri wa miaka 18 amepata ufikiaji wa Huduma bila ruhusa yako, unaweza kuomba data yake ifutwe kwa kuwasiliana nasi kuititia Tovuti yetu ya Ombi

kwenye worldcoin.org/requestportal.

Tukijua kwamba tumekusanya data kumhusu mtoto chini ya umri wa miaka 18, tutafuta data hizo haraka iwezekanavyo. Tumechukua hatua zinazofaa kibashara ili kudhibiti matumizi ya Huduma kwa wale amba wana angalau umri wa miaka 18. Hatutengenezi bidhaa au huduma za sokoni za kununuliwa na watoto.

12. Haki za kisheria chini ya GDPR

Sehemu hii inatumika ikiwa wewe ni mkazi wa Eneo la Kiuchumi la Ulaya. Unaweza kuwa na haki za ziada chini ya GDPR kama ilivyoorodheshwa hapa chini. Ili kutumia haki zako zinazopatikana chini ya GDPR, tafadhali wasiliana nasi kupitia worldcoin.org/requestportal.

- Una haki ya kupata kutoka kwetu wakati wowote unapoomba taarifa kuhusu data ya kibinafsi tunayochakata kuhusu kulingana na Kifungu cha 15 cha GDPR.
- Una haki ya kudai kwamba tusahihishe mara moja data ya kibinafsi inayokuhusu ikiwa si sahihi.
- Una haki, chini ya masharti yaliyoelezwa katika Kifungu cha 17 cha GDPR, ili kudai tufute data ya kibinafsi inayokuhusu. Masharti haya hutoa hasa haki ya kufuta ikiwa data ya kibinafsi haihitajiki tena kwa madhumuni ambayo ilikusanya au kusindika vinginevyo, na pia katika kesi za usindikaji haramu, kuwepo kwa pingamizi au kuwepo kwa wajibu. kufuta chini ya sheria ya Muungano au sheria ya Nchi Mwanachama ambayo tuko chini yake.
- Una haki ya kudai kwamba tuwekee vikwazo uchakataji kwa mujibu wa Kifungu cha 18 cha GDPR.
- Una haki ya kupokea kutoka kwetu data ya kibinafsi inayokuhusu ambayo umetupatia katika muundo uliopangwa, unaotumika kawaida, na unaoweza kusomeka kwa mashine kwa mujibu wa Kifungu cha 20 cha GDPR.
- Una haki ya kupinga wakati wowote, kwa misingi inayohusiana na hali yako fulani, kwa usindikaji wa data ya kibinafsi inayokuhusu ambayo inafanywa, pamoja na mambo mengine, kwa misingi ya Kifungu cha 6 (1) hukumu 1 lit. f GDPR, kwa mujibu wa Kifungu cha 21 cha GDPR.
- Una haki ya kuwasiliana na mamlaka husika ya usimamizi iwapo kuna malalamiko kuhusu usindikaji wa data unaofanywa na mdhibiti. Mamlaka ya usimamizi inayowajibika ni: Ofisi ya Jimbo la Bavaria kwa Usimamizi wa Ulinzi wa Data
- Ikiwa usindikaji wa data ya kibinafsi unategemea idhini yako, una haki chini ya Kifungungu cha 7 cha GDPR ili kubatilisha idhini yako ya kutumia data yako ya kibinafsi wakati wowote na athari kwa siku zijazo, ambapo ubatilishaji ni rahisi kutangaza kama idhini yenyewe. Tafadhali kumbuka kuwa ubatilishaji utaanza kutumika kwa siku zijazo pekee. Uchakataji amba ulifanyika kabla ya ubatilishaji hauathiriwi.

13. Jinsi ya Kuwasiliana Nasi Kuhusu Kauli hii ya Faragha

Unaweza kuamua kufuta data zako kutoka kwenye programu ya Worldcoin. Ikiwa una maswali au wasiwasi zozote kuhusu Kauli hii ya Faragha, ungependa kutumia haki zako, au kuwasiliana na Afisa wa Faragha ya Data (DPO), tafadhali wasilisha ombi lako kupitia Tovuti yetu ya Ombi kwa worldcoin.org/requestportal au kwa kututumia barua kwa anwani, Tools For Humanity Corporation, 548 Market Street, PMB 49951, San Francisco, CA 94104 USA. Tutajibu maombi yote tunayopokea kutoka kwa watu wanaotaka kutumia haki zao za ulindaji data kulingana na sheria husika za ulindaji data. Pia unaweza kufuta data zako kutoka kwenye programu ya Worldcoin.

Iwapo una suala la faragha au matumizi ya data ambalo halijatatuliwa ambalo hatujashughulikia kwa njia ya kuridhisha, tafadhali wasiliana na mdhibiti wa ulinzi wa data katika eneo lako la mamlaka. Unaweza kupata mdhibiti wako wa ulinzi wa data [hapa](#).

